

MATUMAINI PROG NO:2192

TITLE:JAMBO LA KUSHANGAZA.

TEXT:INJILI YA YOHANA 19:31-37.

Hujambo na karibu tujifunze Neno,Leo hii twalichambua neno kutoka injili ya Yohana 19: 19:31-37.

MADA: JAMBO LA KUSHANGAZA.

Jina langu ni David Mungai karibu wimbo halafu tuendele.

WIMBO_____

OMBI_____

Naam nasoma fungu hili la Neno,injili ya Yohana 19: 31-37.

³¹ Basi Wayahudi, kwa sababu ni Maandalio, miili isikae juu ya misalaba siku ya sabato, (maana sabato ile ilikuwa siku kubwa), walimwomba Pilato miguu yao ivunjwe, wakaondolewe.

³² Basi askari wakaenda, wakamvunja miguu wa kwanza, na wa pili, aliyesulibiwa pamoja naye.

³³ Lakini walipomjia Yesu na kuona ya kuwa amekwisha kufa, hawakumvunja miguu;

³⁴ lakini askari mmojawapo alimchoma ubavu kwa mkuki; na mara ikatoka damu na maji.

³⁵ Naye aliyeona ameshuhudia, na ushuhuda wake ni kweli; naye anajua ya kuwa anasema kweli ili ninyi nanyi mpate kusadiki.

³⁶ Kwa maana hayo yalitukia ili andiko litimie, Hapana mfupa wake utakaovunjwa.

³⁷ Na tena andiko lingine lanena, Watamtazama yeye waliyemchoma.

Ilikuwa desturi ya waumini kuvunja miguu ya watu waliosulubiwa ili wafe haraka,lakini walipofika kwa mwili wa Yesu ulikuwa tayari umekufa ili andiko litimie,Daima Mungu ni mwaminifu kutimiza Neno na unabii anaotoa nenoni mwake.

Na vile walivyomchoma na mkuki ilikuwa ili unabii wa Zekaria 12:10 utimie

Nasoma..

¹⁰ **Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza.**

Pia katika ufunuo 1:7 twapata maneno haya.

⁷ **Tazama, yuaja na mawingu; na kila jicho litamwona, na hao waliomchoma; na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. Naam. Amina.**

Kila goti litapigwa mbele ya kiti chake Yesu Kristo maana ndiye atakayotoa hukumu ya mwisho.

OMBI_____

Naam, Endapo wahitaji msaada Zaidi tafadhali wasiliana nasi
anwani na nambari ya

simu ni baada ya wimbo huu.

Wimbo_____

Matumaini

TWR

SLP 21514 CODE 00505

NAIROBI KENYA x2

Simu/Sms 0721970520 x2

Barua Pepe letters@twr.co.ke x2

Jina langu ni David Mungai.

Kwaheri.

End.